

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA



COCAINE



Ujumbe kwa jamii!

1. Wazazi na walezi! wawalee watoto katika maadili mema ikiwemo kuwa nao karibu na kuwasikiliza
2. Vijana wajitambue na kujiepusha na makundi hatarishi yanayoweza kuwaingiza kwenye utumiaji wa sigara, ugoro, pombe, shisha au banga ambavyo watumiaji wengi wa cocaine wanakiri walianza navyo.
3. Usijaribu kuonja cocaine kwani inaleta utaja kwa haraka na ni vigumu sana kuachana navyo.
4. Watumiaji wasinyanyapaliwe waelekezwe kwenye tiba

Wanafunzi
Wanafunzi wengi wanaotumia cocaine hushindwa kuzingatia masomo yao na wengine kushindwa kumaliza shule. Vijana hawa hujikuta hawakubaliki katika jamii zao na kunyanzaliwa hivyo hujitunga na ma-
genge ya wahalifu

Cocacola na cocaine
Kwenye miaka ya 1886 kinywaji cha Coca-Cola kilipoanzishwa kilikuwa na kiasi kidogo cha cocaine. Bada ya madhara ya cocaine kudhhirika katika jamii iliondolewa kwenye Coca-Cola mwaka 1903.

Sheria inasemaje kuhusu cocaine?

Kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015, kujihusisha na cocaine (kusafirisha ndani na nje ya nchi, kuza, kuhifadhi, kusambaza na kutengeneza) ni KOSA LA JINA! na adhabu yake ni kifungo cha maisha.

Utamsaidiaje mtumiaji wa cocaine

Mtumiaji anaweza kupunguza kiasi anachotumia taratibu na hatimaye kuacha. Aidha, asasi za kirala huwasaidia watumiaji kuacha kwa kuwapa unasih! Nyumba za upataji nafuu 'sober house' ambako hupitishwa kwenye hatua 12 za upataji nafuu. Kwa msada zaidi tembelea tovuti www.dcea.go.tz

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya
8 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327,
11486 Dar es Salaam, Tanzania.
Simu+255 22 2113753,
Nukushi:+255 22 2113752
Barua Pepe: cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz

Kimetayarishwa na:

Ni dawa ya kulevya inayotokana na majani ya mmea unaojulikana kitaalam kama Erythroxylum coca ambao hulimwa zaidi kwenye nchi ya Colombia ikifuatiwa na Peru na Bolivia. Asili ya dawa hii ni kuongeza kasi ya utendaji wa mfumo wa fahamu. Watumiaji hutumia cocaine kwa njia ya kunusa, kuvuta, kujidunga au kupaka ambapo huathirika na kuwa wateja wa dawa hiyo. Cocaine huwa katika hali ya unga mweupe au vijive vyeupe. Majina maarufu ya dawa hii yanayotumika mitaani ni pamoja na pele, diego, white sugar na sembe.

Unga wa cocaine na heroin huweza kufanana ingawa heroin hupatikana zaidi kuliko cocaine hapa nchini.

Athari za cocaine

Kiafya:

- ▶ Hufanya mishipa ya damu kusinyaa na kuongeza msukumo la damu na mapigo ya moyo yasiyo na mpangilio hivyo kuleta shinikizo la damu, shambulizi la moyo, kiharusi au kifo cha ghafla
- ▶ Huleta matatizo ya kiakili kama kujihisi unataka kudhuriwa, hasira, ukatili, vurugu, kukosa utulivu na kutaka kujua.
- ▶ Cocaine ikitumika kwa njia ya kunusa husababisha uwezo wa kunusa kupotea, pua kutoboka, mafua yasiyopona na kutoka damu puani
- ▶ Uvutaji wa cocaine ya mawe huharibu mapafu na kupata kikohozi kikali pamoja na kupumua kwa shida



Majani ya coca

- ▶ Cocaine husababisha kusinyaa kwa mishipa ya damu kwenye mfumo wa chakula na utumbo kuoza
- ▶ Cocaine huozesha meno kutokana na ongezeko la asidi na ukavu wa mdomo.
- ▶ Hatari ya maambukizi ya homa ya ini, WU na kifua kikuu kutokana na kushirikiana sindano, kubakwa, biashara ya ngono, kushiriki ngono zembe, kuishi mazingira yasiyo na hewa safi, nk.
- ▶ Cocaine inapokosekana arosto hutokea na kupata uchovu mkali, usingizi, kutetemeka, kuhisi kutambaliwa na vitu mwilini, kutapika, kuwa dhaifu na kushindwa kuwa na utulivu. Arosto pia husababisha kukosa furaha, maumivu makali, kuharisha, homa, kukosa umakini na kuwa na hamu kubwa ya kutumia cocaine
- ▶ Huweza kusababisha vifo kutokana na kuzidisha kiasi cha matumizi
- ▶ Cocaine ikichanganywa na pombe huweza kusababisha kifo.
- ▶ Kukosa usingizi na kuweza kusababisha ajali
- ▶ Kukosa hamu ya kula na kusababisha afya kudhoofu
- ▶ Utumiaji cocaine huchochea uvutaji wa sigara wa mfululizo



Cocaine ya unga



Cocaine ya mawe

Kijamii

- ▶ Mtumiaji kutowajibika na kushindwa kutimiza majukumu katika familia na kusababisha kuvunjika kwa ndoa, kutelekeza watoto na kwa watoto hufukuzwa na kuishi kwenye mageto
- ▶ Ongezeko la vitendo vya uhalifu vikiwemo udokozi, unyang'anyi, utapeli pamoja na mmomonyoko wa maadili (biashara ya ngono).
- ▶ Biashara ya dawa za kulevya huambatana na uhalifu mkubwa kwenye jamii kama ujangili, biashara ya binadamu, biashara haramu ya silaha, utakatishaji fedha, utekaji, ugaidi, madanguro, nk

Kiuchumi

- ▶ Matumizi ya dawa za kulevya hupunguza nguvu kazi ya taifa na kuongeza umasikini kwa familia na jamii kwa ujumla.
- ▶ Biashara ya dawa za kulevya husababisha mzunguko wa fedha haramu, mfumuko wa bei, utakatishaji fedha, kukithiri kwa rushwa na kuongeza tofauti ya kipato
- ▶ Serikali hutumia gharama kubwa kudhibiti tatizo la dawa za kulevya kwenye ukamataji, matibabu, kutoa elimu, nk